

Tanzania, Ng'ombe, Ajira Kwa Watoto

Kuna ushahidi kwamba watoto walio chini ya umri wa miaka 18 wanafuga ng'ombe nchini Tanzania. Kutohakana na uchambuzi wa Uchunguzi Jumuishi wa Nguvu Kazi Tanzania wa mwaka 2020/21, inakadiriwa kuwa watoto 347,957 walio chini ya umri wa kufanya kazi wanafuga ng'ombe. Watoto wanaofanya kazi na mifugo huenda wakawa kwenye mashaka ya kujiweka wazi kwa hatari kadhaa ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa masaa mengi, kujeruhwa na wanyama, na kujiweka wazi kwa athari za hali ya hewa, magonjwa na kemikali kama vile dawa za kuua wadudu. Serikali ya Tanzania inapaswa kupongezwa kwa sababu ya kuendesha na kuchapisha data za uchunguzi zinazosaidia kubuni na kutekeleza sera na programu madhubuti za kukabiliana na ajira kwa watoto.